Umoja wa Mataifa Swahili **S**/RES/1325 (2000)

# Baraza la Usalama

Isambazwe kwa watu wote
31/10/04

**Pendekezo nambari** 1325 (2000)

**Lililokubaliwa na Baraza la Usalama katika mkutano wake wa 4213 uliofanyika tarehe 31/10/2000.**

*Baraza la Usalama*

*Linayarejea* mapendekezo yake nambari 1261 ya (1999) tarehe 25/8/1999, pendekezo nambari 1265 la (1999) tarehe 17/9/1999, pendekezo nambari 1296 la (2000) tarehe 19/4/2000 na pendekezo nambari1314 la tarehe 11/8/200, pia taaarifa ya Rais wake (wa Baraza la Usalama) zinazohusiana na mapendekezo hayo. Na inairejea taarifa ya Raisi wake kwa vyombo vya habari aliyoitoa kuadhimisha Siku ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Wanawake na Siku ya Amani Duniani (Siku ya Wanawake Duniani) ya tarehe 8/3/2000,
(SC/6816),

*Kadhalika linarejea* ahadi zake za kutekeleza Azimio la Beijing pamoja na mipango ya utekelezaji wake (A//52/231) na yale yaliyomo kwenye waraka wenye matokeo ya Kikao Maalumu cha ishirini na tatu cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kinachoitwa “Wanawake mwaka 2000: Usawa wa Kijinsia, Maendeleo na Amani katika Karne ya Ishirini na Moja.” (AS-23/10/Rev.1), hasa yale makubaliano juu ya wanawake kwenye mapambano ya vita**,**

*Kwa kuzingatia* malengo na misingi ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa, na jukumu la kwanza la Baraza la Usalama kufuatana na Mkataba wa kudumisha usalama na amani duniani,

Li*meonesha* wasi wasi wake juu ya raia, hasa wanawake, na watoto ambao wengi wao ndio wanaoathirika na migogoro ya vita, pamoja na wakimbizi, na wale waliomo nchini ambao wamekimbia makazi yao, na ambao wanalengwa zaidi na wapiganaji na watu wenye silaha, kadhalika inatambua matokeo yake katika kuleta amani na upatanishi wa kudumu,

*Linatilia mkazo* jukumu muhimu la wanawake katika kuepusha na kusuluhisha migogoro, na kuleta amani, vilevile linasisitiza umuhimu wa wanawake kushirikishwa kwa usawa na kuhusishwa kikamilifu katika juhudi zote za kuleta na kuendeleza amani na usalama, pamoja na haja ya kuwapa fursa zaidi katika kufanya maamuzi yanayohusiana na uzuwiaji na upatanishi wa migogoro,

*Kadhalika linasisitiza* haja ya kutekeleza kikamilifu Sheria ya Kimataifa ya kuhurumia binaadamu na sheria inayohusu haki za binadamu ambayo itahifadhi haki za wanawake na wasichana wakati na baada ya migogoro,

*Linasistiza* kwa wote walio husika haja ya kuhakikisha kwamba kuondolewa kwa mabomu yaliyotegwa ardhini na mipango ya kuwahamasisha watu kuhusu mabomu hayo inazingatia mahitaji mahasusi ya wanawake na wasichana,

*Linatambua* haja ya kuharakisha masuala ya kijinsia yaeleweke katika shughuli za kuleta amani, huku kukizingatiwa Azimio la Windhoek na Mpango wa Namibia wa Kutekeleza uwelewano wa kijinsia kwa wote katika Shughuli za Viikosi Mbali Mbali Vya Kuchangia Amani. (S/2000/693),

*Vile ville linatambua* umuhimu wa pendekezo liliyomo katika taarifa ya Rais wake kwa vyombo vya habari aliyoitoa tarehe 8/3/04 kuwa vikosi vyote vya kulinda amani vipatiwe mafunzo maalumu juu ya hifadhi, mahitaji mahasusi na haki za binaadamu kwa wanawake na watoto kwenye mazingira ya migogoro,

*Linatambua* kuwa kueleweka kwa athari za migogoro kwa wanawake na wasichana, mipango madhubuti itayofanywa na taasisi kuhakikisha hifadhi yao pamoja na kuwashirikisha kikamilifu katika utaratibu wa kuleta amani inaweza kuchangia pakubwa kuleta na kuendeleza amani na usalama ulimwenguni,

*Linatanbua* haja iliopo ya kuimarisha taarifa juu ya athari za mapambano ya kivita kwa wanawake na wasichana,

1. *Linahimiza* Nchi Wanachama kuhakikisha uwakilishi zaidi wa wanawake katika maamuzi ya taasisi za kitaifa, kimikoa na za kimataifa, na kwenye mipango ya kuzuia na kusimamia usuluhishaji wa migogoro;

2. *Linampa moyo* Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa katika kutekeleza mikakati yake (A/49/587) inayotaka kuongezwa kushirikishwa kwa wanawake katika maamuzi na usuluhishaji wa migogoro na utaratibu wa kuleta Amani;

3. *Linamhimiza* Katibu Mkuu wa Umoja Mataifa kuteuwa wanawake zaidi kama wawakilishi na wajumbe maalumu ili kutekeleza mipango kikamilifu kwa niaba yake, vivyo hivyo linazitaka Nchi Wanachama zipendekeze wanawake kwa Katibu Mkuu, ili majina yao yasajiliwe katika orodha kuu ambayo hupitiwa kila mara;

4. *Vilevile linamhimiza* Katibu Mkuu afanye bidii ya kuongeza nafasi na mchango wa wanawake katika shughuli za Umoja wa Mataifa zinazotendeka sehemu mbalimbali, hasa kwa wachunguzii wa shughuli za kijeshi, askari polisi, na watu wanaoshughulika na haki za binaadamu na wanaotoa huduma za misaada;

5. *Lienyoshe liko* tayari kuzingatia wa masuala ya kijinsia katika shughuli za vikosi vya kulinda amani, linamhimiza Katibu Mkuu kuhakikisha kwamba, kila ipasapo, mambo ya kijinsia yawemo kwenye shughuli za sehemu mbalimbali;

6. *Linamuomba* Katibu Mkuu azipatie Nchi Wanachama miongozo ya mafunzo na vyombo vya kufundishia juu ya hifadhi, haki na mahitaji mahasusi ya wanawake, pamoja na umuhimu wa kuwashirikisha wanawake hao katika hatua zote za kuleta na kudumisha amani, linazitaka Nchi Wanachama zishirikishe masuala hayo pamoja na mafunzo ya kuwaelemisha watu juu ya UKIMWI katika mipango yao ya kitaifa ya mafunzo kwa wanajeshi na polisi, kwa ajili ya matayarisho ya kupelekwa kwenye sehemu zinazohitajika, zaidi linamuomba Katibu Mkuu ahakikishe kuwa mafunzo hayo hayo wanapatiwa raia wanaofanya kazi katika vikosi vya kulinda amani;

7. *Linazihimiza* Nchi Wanachama zijitolee zaidi kuchangia, kifedha, kiteknolojia na kutoa msaada unaohitajika kwa ajili ya juhudi za mafunzo ya masuala ya kijinsia, ikiwa ni pamoja na yale yanayofanywa kwa misaada ya fedha na miradi inayohusika, kwa mfano, Msaada wa Fedha wa Umoja wa Mataifa kwa ajili ya wanawake, Msaada wa Fedha wa Umoja wa Mataifa kwa ajili ya watoto, na yale yanayofanywa na Shirikisha la Wakimbizi ya Umoja wa Mataifa , pamoja na mashirika mengineyo yanayohusika;

8. *Linawataka* wote wanaohusika pale wanaposhauriana na kutekeleza makubaliano ya kuleta amani, wazingatie masuala ya kijinsia, yakiwemo, kwa mfano:

(a) Mahitaji mahasusi ya wanawake na wasichana wakati wa kuwarudisha makwao na kuwatafutia makazi, na kuwatayarisha na maisha baada ya vita,

(b) Hatua zinazounga mkono juhudi za wanawake wenyewe katika kuleta amani, na juhudi za jadi za kusuluhisha migogoro, na kwamba kuwahusisha wanawake katika kusimamia utaratibu kutekeleza makubaliano ya kuleta amani,

(c) Hatua ambazo zitahakikisha hifadhi na kuheshimu haki za binaadamu za wanawake na wasichana, hasa zile zinazohusiana na katiba, mfumo wa upigaji kura, idara za polisi na vyombo vya sheria;

9. *Linawataka* wote waliohusika na migogoro ya vita kuheshimu kikamilifu Sheria ya Kimataifa inayowapa haki na hifadhi wanawake na watoto wa kike, kama raia, na hasa wayatimize yale majukumu yanayowahusu wao chini ya Makubaliano ya Geneva ya 1949 na zile Kanuni zZiada zilizofuatia 1977, Makubaliano ya Masuala ya Wakimbizi ya 1951 na Kanuni zilizofuatia 1967, Makubaliano ya Kukomesha Ubaguzi wa Aina Yoyote Kwa Wanawake ya 1999, na zile Kanuni Mbili za Hiari zilizofuatia tarehe 25/5/2000, pia wazingatie vifungu vilivyomo kwenye Mkataba wa Rome wa Mahakama Ya Kimataifa ya Kesi za Jinai;

10. *Linawataka* wote waliohusika na vita wachukue hatua maalamu ili kuwahifadhi wanawake na wasichana kutokana na maovu wanayotendewa kwa sababu ya jinsia yao, hasa kunajisiwa na aina nyingine za kubughudhiwa kijinsia, pamoja na vitendo vyote vyenye kutumia nguvu wakati wa vita;

11. *Linasisitiza* jukumu la Nchi zote kuacha kuwasemehe, na badala yake kuwashtaki wale wanaohusika na mauaji halaiki, Uhalifu Dhidi ya Ubinaadamu, na Uhalifu wa kivita ikiwa i pamoja na uhalifu wa kunajisi, na wowote ule dhidi ya wanawake na wasichana, na kutokana na hayo *linasisitiza* umuhimu wa kuondoa uhalifu kama huo, katika vifungu vya vya makosa yanayopewa msamaha;

12. *Lintoa wito* kwa wote wanaohusika na vita waheshimu raia na waheshimu nidhamu za utoaji huduma katika kambi na makazi ya wakimbizi, wazingatie mahitaji mahasusi ya wanawake na wasichana, ikiwa pamoja na mipango yao, *na linarejea* maazimio yake nambari 1208 (1999) tarehe 19/11/98 na nambari 1296 tarehe 19/4/2000;

13. *Linawahimiza* wote wanaohusika na mipango ya kusalimisha silaha na ile ya kuwasaidia watu warejee kuishi katika jamii kuzingatia mahitaji tofauti ya wapiganaji wa kike na wa kiume, na kungalia mahitaji ya wale wanaowategemea;

14. *Linathibitisha* kwamba liko tayari, kila hatua zinapopendekezwa, kufuatana na Ibara ya 41 ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa , kwamba litaangalia athari zinazoweza kutokea kwa raia, likizangatia mahitaji mahasusi ya wanawake na wasichana, ili kutoa msamaha muwafaka na wa kibinaadamu;

15. *Limetoa kauli yake kuwa* litahakikisha kwamba Uwakilishi wa Baraza la Usalama unayafikiria masuala ya kijinsia na haki za wanawake, pamoja na kushauriana na vikundi vya wanawake vya kitaifa na vya kimataifa;

16. *Limependekeza* kuwa Katibu Mkuu afanye utafiti juu ya athari za vita kwa wanawake na wasichana, mchango wa wanawake katika kuleta amani pamoja na masuala ya kijinsia katika utaratibu wa kuleta amani na usuluhishaji wa migogoro, kadhalika limependekeza

awasilishe ripoti ya matokeo ya utafiti huo kwa Baraza la Usalama, na atoe matokeo yake kwa Nchi zote Wanachama wa Umoja Mataifa;

17. *Linamuomba* Katibu Mkuu, pale inapostahiki, aelezee katika ripoti yake kwa Baraza la Usalama maendeleo kuhusu kuleta uwelewano wa kijinsia katika shughuli zote za kulinda amani, na mengineyo yanayohusiana na wanawake na wasichana;

18. *Baraza la Usalama limeamua* kufanikisha kwa dhati masuala yote.